

Madrid 02/07/2010

Toka: Kamati ya kuratibu mkutano wa kimataifa LMC (WAMISCO)

Kwa: Jumuiya zote za WAMISCO za Marekani, Africa, Ulaya

Ndugu Wapendwa,

Salaam. Tunawaandikieni kwa niaba ya jumuiya za WAMISCO zilizopo Ulaya ili kuwaleteeni pendekezo la kuwa na mkutano wa WAMISCO kimataifa. Baada ya mikutano iliyofanyika Ulaya (Lisbon 2007, Lisbon 2008, Madrid 2010) Africa (Kenya 2009) na Marekani (San Paolo 2010) tumefikiri kwamba wakati umefika wa kuota ndoto ya kuwa na mkutano wa WAMISCO wa mabara yote.

Madhumuni maalum za mkutano huo ni kama ifuatavyo:

- ✓ Kufahamiana, kushirikishana hali halisi, na kuona tumefikia wapi katika Regions mbalimbali tulipo
- ✓ Kwa vile mikutano mikuu (General Chapters) ya IMC na MC itafanyika mwaka 2011 kuwafamisha vizuri washiriki kuhusu safari yetu mpaka sasa katika mabara yote, na kuwafamisha kuhusu roho ya kifamilia inayotuunganisha, ingawa tunaishi katika mazingira tofauti tofauti
- ✓ Kutembelea mahali pa kihistoria pa Familia ya Consolata (alipozaliwa na kuishi Baba Allamano na alipoanzisha mashirika yake ya kimisionari)

Ni pendekezo letu mkutano ufanyike Italia kati ya tarehe 01/09/2011 – 01/16/2011. Ratiba inafikiria siku kadhaa Torino na siku kadhaa Roma. WAMISCO wa Ulaya, kadiri inavyowezekana, watajitahidi kusaidia, hasa katika wikendi ya 01/14/2011 – 01/16/2011.

Ni vema angalau mjumbe 1 (ikiwezekana 2) kutoka kila Region ashiriki, akichaguliwa kati ya WAMISCO wazalendo, na mwanakundi kamili.

Katika maandalizi ya mkutano huu wa kimataifa itabidi kila Region itayarishe ripoti kuhusu hali halisi ya WAMISCO ikizingatia vipengele vifuatavyo:

- ✓ Historia ya WAMISCO katika Region
- ✓ Jumuiya zilizopo na idadi ya wana WAMISCO
- ✓ Muundo (organization) wa kiRegion au kibara wa WAMISCO
- ✓ Shughuli zinazotendeka nchini (kuhamisha roho ya kimisionari, haki na amani, mitindo (styles) ya maisha)
- ✓ Shughuli zinazofanyika nje ya nchi (WAMISCO kutumwa nchi nyingine)
- ✓ Mipango ya kiRegion kwa miaka 3 ijayo

Ili kurahihisha maandalizi ya tukio hilo tunaomba mtujulishe kuhusu uwezekano wa mjumbe 1 au 2 kushiriki mkutano huo. Tutafikiria jinsi ya kusaidia walio na shida ya kiuchumi ili kuwezesha Regions zote kushiriki.

Mapema yawezekanavyo kwenye internet, www.ismico.org chini ya kipengele LMC, tutaweka programu, barua ya mwaliko, fomu ya kujiandikisha na taarifa husika. Kwa maswali, mapendekezo na yote mintarafu mkutano huo mtaweza kuwasiliana na wafuatao:

- ✓ Pd. Paco Lopez, mshauri mkuu kwa bara la Ulaya na Asia
- ✓ Sista Cesariana Corioni, cesariana.mc@gmail.com
- ✓ Diego Aguilar, Italia: diego.agui@libero.it

Tunawatakieni Kwaresima njema, tukiwa na matumaini kwamba kwa kila mmoja wetu itakua kweli wakati mwafaka wa kumgeukia Mungu. Pia ni tumaini letu kwamba sherehe ya Pasaka itatuletea furaha ya Bwana Mfufuka. Tunatarajia kupata maoni yenu, mapendekezo yenu na kujiandikisha kwenu.

Tunawaaga katika amani na faraja.

Ni sisi wanakamati ya kuratibu mkutano wa kimataifa, WAMISCO